



Umma wa Wapanda Baisikeli Dar es Salaam  
(UWABA)  
Manzese Sisi kwa Sisi  
PO Box 90361  
Dar es Salaam

NGO Registration Number 02NGO/0683  
[www.uwaba.or.tz](http://www.uwaba.or.tz)  
email: [uwabadar@yahoo.co.uk](mailto:uwabadar@yahoo.co.uk)  
+255 713 652642 / +255 715 568512

19 July 2010

Commander Mpinga  
Mkuu wa Traffic Police  
Dar es Salaam

**YAH: MAWAZO KUHUSU TANGAZO LA REDIO LA TRAFFIC POLICE  
KUHUSU SHERIA ZA KUEGESHA MAGARI**

UWABA tunashukuru kupata nakala ya tangazo la redio liliyotayarishwa na Traffic Police kutangazwa kwenye Radio Uhuru FM.

Sehemu mbali mbali za tangazo hili zinaweza kuboresha usalama kwa wapanda baisikeli na watembea kwa miguu, mfano:

- “Ni makosa na unastahili kuchukuliwa hatua za kisheria endapo utakutwa umeegisha gari au kupakia na kushusha mizigo kwenye njia ya waendao kwa miguu. Mfano Uhuru Rd. maeneo ya kwanzia shule ya Uhuru mpaka clocktower mnara wa saa.”
- “Kabla ya wewe dereva au abiria wako kufungua mlango, hakikisha hutamgonga mtu yeyote anayepita barabarani au kwenye njia ya watembea kwa miguu, waendesha baisikeli pikipiki.”
- “Usipaki pasipo alama ya parking au mistari ya njano kwenye kingo za barabara.”
- Usipaki “Barabara yenye mistari myeupe miwili ya katikati hata kama moja ya mistari hiyo imekatikakatika”
- “Usiegeshe mahali popote ambapo itakuwa hatari au kusababisha matatizo kwa watumiaji wengine wa barabara”

UWABA tunashukuru kwamba maelezo haya yamewekwa kwenye tangazo ili kuongeza usalama kwa watembea kwa miguu na wapanda baisikeli.

Tuna mapendekezo na maswali haya:

- tunapendekeza kwamba tangazo lisemi rasmi kwamba ni marufuku kuegesha magari kwenye service road
- tunaona kwamba barabara chache zina mistari ya njano miwili. Tunaomba kujua ni shirika gani la serikali ambalo lina majukumu kuweka mistari hii.
- Tunaomba sheria itekelezwe na madereva wa magari wanaoegesha magari kwa kutofuata tangazo hili wakamatwe na wapigwe faini. Tunaona kuna magari mengi kwenye service roads mfano Morogoro Road Manzese na Nelson Mandela Road pia kuna traffic police karibu lakini hawachukui hatua.

Tunaomba kuendelea kupata taarifa kutoka kwa Traffic Police kuhusu matangazo kama haya na hatua zinazochukuliwa kutekelezwa sheria hizi.

Wako katika ujenzi wa Taifa

Fredrick (Mejah) Mbuya  
Mwenyekiti UWABA